Mpango wa Chanjo la Kovid-19: Ukurasa huu unashughulikia wasiwasi wako

Toleo la 7 - 17.03.2021

Chanjo hili litanipa Kovid-19?

Chanjo yenyewe haiwezi kukuletea Kovid-19. Utakapopokea dozi zote mbili za chanjo ndipo utapunguza uwezekano wakuathirika zaidi na ugonjwa huu katika siku za badaaye.

Kama nimekuwa na Kovid-19, je, ninahitaji kupewa chanjo? Vipi kama nina, au nimekuwa na 'Kovid ya muda mrefu'?

Hatujui kama kuwa na Kovid-19 inakulinda dhidi ya kushikiwa na ugojwa huu tena, lakini tunahimiza kila mtu apate chanjo anapoalikwa kufanya hivyo.

Ikiwa una dalili ambazo zinafana na za virusi vya Korona unapaswa kupimwa kabla na huwezi kupata chanjo yako hadi kipindi chako cha kujitenga kiishe.

Mahali ambapo watu wanakabiliwa na matatizo makubwa yanayoendelea kutokana na Ugonjwa wa Virusi vya Korona (COVID-19), watu wanapaswa kuzungumza na daktari ili kujua kama watapata chanjo wakati huo.

Je chanjo inafanyaje kazi, na inafanya kazi kwa muda gani?

Chanjo hufanya kazi kwa kutengeneza protini kutokana na virusi ambavyo ni muhimu kwa kujenga kinga ya mwili.

Protini hufanya kazi kwa njia ile hufanya katika chanjo zingine kwa kuchochea mfumo wa kinga, ili kutengeneza antibodi na seli za kupambana na maambukizo.

Tunatarajia chanjo hili litafanya kazi angalau kwa mwaka mmoja – ikiwa haitakuwa kwa muda mrefu zaidi. Haya yatafuatiliwa mara kwa mara.

NHS [NHS -wizara ya afya] inauhakika chanjo liko salama?

Ndiyo. NHS haiwezi kotoa chanjo zozote za Kovid-19 kwa umma hadi wataalamu huru wanaposaini kuwa iko salama kutumiwa.

MHRA, [MHRA-shirika la kudhibiti madawa] mdhibiti rasmi wa Uingereza, amesema chanjo hizi ziko salama na zina ufanisi mkubwa.

Kama inavyokuwa na dawa zote, chanjo hukaguliwa katika kila hatua katika mchakato wa maendeleo, na viwanda hufuatiliwa mara tu zimeidhinishwa na zinatumika kwa idadi kubwa ya watu.

Je, kuna madhara yoyote?

Madhara ni jambo muhimu ambayo MHRA daima wanazingatia wakati wa kupima chanjo zote kabla wakubali zitumiwe.

Kwa chanjo za Covid-19, kama ilivyo kwa zingine nyingi, wamebaini kuwa baadhi ya watu wanaweza kujisikia vibaya kidogo, lakini wanaripoti kwamba hakuna madhara makubwa yamezingatiwa katika makumi ya maelfu ya watu waliojihusisha na majaribio yake.

Unapopata chanjo la Kovid-19, kunauwezekano wa kupata na madhara kiasi. Haya yanaweza kuwa ni jumuia ya yaliotanjwa hapa chini:

- Kidonda mkononi ambapo sindano limeingilia
- kuhisi uchovu
- maumivu ya kichwa
- kuhisi muacho

Ikiwa ni hivyo unaweza kuchukua dawa za maumivu, kama vile paracetamol, ikiwa unahitaji. Kama dalili zako zitazidi kuwa baya au uwe na wasiwasi, piga simu nambari 111.

Maelezo zaidi juu ya madhara yanaweza kupatina kwa tovuti: https://www.nhs.uk/conditions/coronavirus-covid-19/coronavirus-vaccination/coronavirus-vaccine/

Vipi kuhusu mzio ambao umeripotiwa?

Chanjo za Kovid-19 ni salama na linafaa kwa idadi kubwa ya watu – Dawa hizo zimejaribiwa kwenye makumi ya maelfu ya watu na kupimwa na wataalamu.

Mtu yeyote mwenye historia ya mzio wa haraka [anaphylaxis] kwa viambato ziliyomo kwenye chanjo hapaswi kuzipokea.

Dozi ya pili ya chanjo ya Pfizer / BioNTech haipaswi kutolewa kwa wale ambao wamepata mzio wa haraka [anaphylaxis] kwa dozi ya kwanza ya chanjo ya Pfizer / BioNTech.

Kila mtu ataulizwa maswali ili kuona kama anaweza kuwa na mzio kabla ya kupata chanjo.

Wafanya kazi wa chanjo wote wana mafunzo yanayohitajika ili kukabiliana na matokeo yoyote adimu kutokana na mzio, na kumbi zote za chanjo zitakuwa na vifaa vya kuwahudumia watu watakapozihitaji - kama tu vile kwa chanjo zingine zote hua.

Chanjo inaweza kubadilisha nyenzo zako za maumbile?

Hakuna ushahidi wa kupendekeza kwamba kuwa na chanjo ya Kovid-19 itabadilisha nyenzo za maumbile ya mtu anayeipokea.

Chanjo ya Covid-19 huathiri rutuba?

Hakuna ushahidi kwamba chanjo ya Covid-19 inathiri rutuba.

Naweza kupata chanjo kama nina mimba au ninanyonyesha?

Ndiyo. MHRA [MHRA-shirika la kudhibiti madawa] limesasisha mwongozo wao wa kusema kuwa wanawake wajawazito na wale wanaonyonyesha wanaweza kupata chanjo hiyo lakini wanapaswa kuijadili jambo hilo na na daktari ili kuhakikishwa kuwa faida zinazidi hatari zozote zinazoweza kujitokeza.

Chanjo zitafanya kazi na matatizo mapya ya virusi vya Korona?

Hakuna ushahidi kwa sasa kwamba chanjo haitafanya kazi dhidi ya matatizo mapya ya Kovid-19, na kwa hivyo tunaendelea kutoa chanjo kwa watu kama kawaida. Wanasayansi wanaangalia kwa undani jinsi virusi vinavyoathirishwa na chanjo hizo. Virusi, kama vile vinasababisha homa ya majira ya baridi, mara nyingi hujigawa kuwa tawi na huleta matatizo tofauti ambazo lakini katika mara chache tu huzuia chanjo kufanya kazi.

Chanjo zina ufanisi kiasi gani? Zinachukua muda gani kufanya kazi?

MHRA [MHRA-shirika la kudhibiti madawa] wamesema chanjo hizi zina ufanisi mkubwa, lakini ili kupata ulinzi kamili mwilini watu wanahitaji kurudia dozi ya pili – hii ikiwa ni muhimu sana.

Ili kuhakikisha watu wengi wanachanjwa haraka iwezekanavyo, Idara ya Huduma za Afya na Jamii sasa inashauri kwamba dozi ya pili ya chanjo ya OxfordAstraZeneca na chanjo ya Pfizer/BioNtech inapaswa kupangiwa iwe baada ya wiki 12 mbali.

Kinga kamili huanza baada ya karibu wiki moja au mbili baada ya dozi hiyo ya pili, na ndiyo sababu ni muhimu unapoalikwa, fanya miandi haraka iwezekanavyo. Hata wale ambao wamepokea chanjo zote mbili bado wanahitaji kufuata taratibu za kuangalia umbali katika jamii na maongozo mengine.

Kwa nini ninahitaji dozi zote mbili za chanjo ya Kovid-19?

Chanjo ya Kovid-19 hutolewa kwa dozi 2, na ni muhimu kupata zote mbili. Mwili wako hujenga kinga bora kwa dalili za Kovid-19 wakati chanjo inatolewa kwa dozi mbili, ndogo, na kunakuwa na wakati katikati ya chanjo hizo mbili.

Ushauri mpya kutoka kwa Maafisa Wakuu wa Matibabu ya Uingereza ni kwamba dozi ya pili ya chanjo hiyo bado inafaa wakati ikitolewa iwe ni hadi wiki 12 baada ya dozi ya kwanza, na inapaswa kutolewa mwishoni mwa kipindi hiki cha wiki 12.

Hii itasaidia kuhakikisha kuwa watu wengi kama iwezekanavyo wanafaidika na dozi ya kwanza ya chanjo kwa njia ya haraka sana. Hakuna wasiwasi wa usalama kwa watu tayari wamekuwa na dozi yao ya pili mapema zaidi ya wiki 12 baada ya dozi yao ya kwanza.

Chanjo zilitengenezwa vipi haraka sana?

Kuna sheria kadha za utumianji wa madawa, zikiwa ni pamoja na za chanjo, ambazo zimeundwa, za kupima na zinapatikana kwa umma - na hizo si tofauti kwa chanjo zilizoidhinishwa za KOVID-19.

Kuna sababu kadhaa ambazo ziliwezesha kuendeleza chanjo za Kovid-19 haraka ikilinganishwa na dawa zingine;

1. Chanjo hutengenezwa kwa njia ya kupimwa katika awamu tofauti; awamu za upimaji wa chanjo za Covid-19 ziliendeshwa kwa wakati mmoja au kupishana, ambazo zilichukua mchakato.

2. Takwimu kutoka vipimo zilipatikana haraka na kuezesha wataalamu wa MHRA kupitia vipimo vilivyokuwa vikitolewa kwa kuuliza maswali wakati wanapoendelea, na sio kama kawaida wanapopata taarifa zote hapo mwishoni mwa kipindi cha upimaji.

3. Majaribio ya kliniki ya chanjo ya Covid-19 yaliweza kuwahusisha watu haraka sana kama juhudi za kimataifa zilimaanisha maelfu ya watu walikuwa tayari kujitolea.

Chanjo imejaribiwa na watu kutoka asili tofauti za kikabila, na pia watu kutoka kwa vikundi vya magonjwa ya 'hatari kubwa' au ya muda mrefu?

Ripoti za tathmini za umma zina taarifa zote za kisayansi kuhusu majaribio na taarifa juu ya washiriki wa majaribio.

Kwa jaribio la Pfizer, washiriki walijumuisha 9.6% watu weusi wa Kia-Afrika, 26.1% Hispania na Latino, na 3.4% wa Ki-Asia. Kwa chanjo la Oxford / AstraZeneca 10.1% ya wapokeaji wa majaribio walikuwa watu weusi na 3.5% wa Ki-Asia.

Hakuna ushahidi wowote wa chanjo hizo zinafanya kazi tofauti katika makundi tofauti ya kikabila.

Kwa chanjo zote mbili, watu waliohusika katika majaribio hayo walikuwa wanatoka katika umri wa miaka mbalimbali, pamoja na wale walio na hali baya za afya. Majaribio yote mawili ya chanjo yaligundua yakuwa yalikuwa na mafanisi bora kwa watu katika makundi haya.

Maelezo ya washiriki wa majaribio kwa chanjo zote mbili huchapishwa mtandaoni.

Habari ya chanjo ya Pfizer/BioNTech inapatikana katika tovuti: https://www.gov.uk/government/publications/regulatory-approval-of-pfizer-biontech-vaccine-for-covid-19

Kwa taarifa ya chanjo ya Oxford/AstraZeneca inapatikana hapa: https://www.gov.uk/government/publications/regulatory-approval-of-covid-19-vaccine-astrazeneca

Siwezi kutumia baadhi ya dawa kwa sababu ya imani yangu au mahitaji ya lishe. Viambato vya chanjo vina nini?

Chanjo ya Covid-19 haina bidhaa zozote za wanyama au za yai.

Viambato vyote huchapishwa katika taarifa za huduma ya afya kwenye tovuti ya MHRA kwenye mt hapo juu.

Mimi ni sehemu ya jamii ya Waislamu na nina wasiwasi na kupokea chanjo – ninawezaje kujua zaidi?

Jumuiya ya Matibabu ya Kiislamu hapa Uingereza limetoa ushauri mahususi unaowatakia Waislamu wanaomchunguza Ramadhani kutochelewesha kupata chanjo hiyo, na kutoa

uchambuzi kutoka kwa wanazuoni wa Kiislamu ambao unasema kuwa sindano za madhumuni yasiyo ya lishe hazibatilisha mfungo.

Taarifa kuhusu mpango wa chanjo zinapatikana

- Tovuti ya Baraza la Waislamu la Uingereza, na
- Jumuiya ya Matibabu ya Kiislamu ya Uingereza.

Je, nitapewa chaguo kuhusu kupokea chanjo? Naweza kuchagua ni aina gani ya chanjo nitayopokea?

Unaweza kuchagua kutopata chanjo ya Covid-19 au kutopata; hata ikiwa ni hivyo, NHS inahimiza kila mtu apate. Vile idadi ya watu wengi watakapopata chanjo, ndivyo vitakuwa vigumu kwa virusi kuenea. Haitawezekana kuchagua kati ya chanjo tofauti kwa jinsi njia za kuhifadhi ni dogo, lakini hata ikiwa hivyo ni muhimu kutumia ile inaopatikana wakati wako.

Kama nimepata chanjo ya Covid-19, bado ninaweza kuambukiza watu wengine?

Chanjo ya Covid-19 inapaswa kukulinda dhidi usiwe mgonjwa, lakini haitakuzuia kuambukiza watu wengine. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba uendelee kukumbuka hali ya kuweka mikono, uso, na umbali. Nawa mikono yako, funika uso wako na umbakishe umbali wako kutoka kwa watu wengine.

Naweza kupata chanjo kama sina Namba ya NHS?

Ndiyo. Watu hawahitaji nambari ya NHS au usajili wa GP [Daktari wa familia] kupokea chanjo na kamwe hawapaswi kukataliwa moja kwa msingi huu. Viongozi wa eneo hilo wametakiwa kuchukua hatua kuhakikisha hii isi endeleshwe.

Ikiwa mtu hana nambari ya NHS lakini yuko ndani ya kikundi anayestahiki, huduma zimeshauriwa kutoa chanjo sasa, rekodi ndani kupitia mfumo wa karatasi, na kuhakikisha chanjo inarekodiwa rasmi baadaye.

Unaweza kupata nambari yako ya NHS kupitia tovuti ya NHS. Utaombwa otoe jina lako, tarehe ya kuzaliwa na msimbo wa posta, na nambari yako ya NHS itakutumia, barua pepe au barua ya mandiko.

Mtu yeyote anaweza kujiandikisha katika kituo cha GP [Daktari wa familia] - haihitajiki uthibitisho wa anwani au hali ya uhamiaji.

Kwa habari za hivi sasa kuhusu mahali yaliopangwa ya kutoa Chanjo ya Covid-19 soma- www.norfolkandwaveneyccg.nhs.uk/covid-19-vaccination-programme